**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA UFUNDI STADI VETA CHATO**

---

**REF. NO. CDVTC/CT/TG.60/15/01** **Tarehe: 05/12/2023**

…………………………………………….

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA UFUNDI STADI CHATO – 2024 – (LEVEL I)</u>**

## 1. UTANGULIZI

Uongozi wa chuo na jumuiya yote ya chuo cha ufundi stadi VETA CHATO, unakupongeza na kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Chuo cha ufundi stadi VETA CHATO, katika fani ya …………………………………………………………… ambapo utaishi ………………………(KUTWA/BWENI). Nafasi hii ni adimu Sana, hata hivyo wewe umekuwa miongoni mwa vijana wachache waliobahatika kupata nafasi miongoni mwa wengi walioomba. Ni matumaini yetu kuwa utaitumia vema nafasi hii, katika kipindi chako cha mafunzo ili uweze kujijengea maarifa, stadi na mwelekeo wa kutosha kukidhi mahitaji ya kuwa fundi stadi wa sasa na baadae.

Mafunzo ya ufundi stadi yameandaliwa kwa lengo la kuwajengea umahiri kitaaluma, na katika stadi za kazi katika misingi ya kwenda kuajiriwa au kujiajiri baada ya kuhitimu.

## 2. MAHALI CHUO KILIPO NA JINSI YA KUFIKA CHUONI

**a) Mahali chuo kilipo**

Chuo cha ufundi stadi VETA CHATO, kipo Mkoani Geita, Wilaya ya CHATO katika kijiji cha ITALE, pembezoni mwa barabara iendayo Geita ukitokea Bukoba, umbali wa kilometa nne kutoka CHATO mjini.

**b) Jinsi ya kufika chuoni**

Kama utakuwa unatokea barabara itokayo Geita unaweza kushukia chuoni moja kwa moja au kushuka stendi ya mabasi Chato na kisha ukakodi usafiri wa pikipiki au bajaji kufika Chuoni.

**c) Hali ya hewa na mazingira ya chuo.**

Mazingira na hali ya hewa Chuoni CHATO ni ya joto la wastani mchana, na baridi kidogo nyakati za jioni. Kwa hali hii wanachuo hawalazimiki kubeba nguo za kujikinga na baridi kali wajapo chuoni. Pia mwanafunzi hawapaswi kuja na nguo nyingi ambazo sio sare (zisizidi mbili), nguo za kubana(skin tight) haziruhusiwi kabisa.

3. **MAELEKEZO KWA AJILI YA USAJILI**

I. Chuo kitafunguliwa tarehe **15/01/2024.** Mafunzo yatachukua muda miaka miwili kwa (level I) na miaka mitatu kwa atakayesoma hadi (level III). Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **26/01/2024**.

II. Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uje na kitambulisho, nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala za vyeti vyako vya kitaaluma, pamoja na barua hii.

III. Unatakiwa uje na cheti cha Daktari wa hospitali inayotambuliwa na Serikali kuthibitisha kuwa una afya njema ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa. (Fomu ya vipimo imeambatanishwa).

IV. Unatakiwa ufike na picha tatu za pasipoti (Passport size)

V. Unatakiwa kuthibitisha wewe pamoja na mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo katika fani uliyo pangiwa.

VI. Mwanachuo hatapokelewa Chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vipengele II-V vilivyotajwa hapo juu.

4. **ADA**

Ada ya mafunzo ni **Tshs. 120,000/=** kwa Mwanafunzi wa **BWENI** au **Tshs. 60,000/=** kwa Mwanafunzi wa **KUTWA** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa mara moja au kwa awamu kulingana na mhula ya masomo. Malipo haya yafanyike kwa kutumia control number ambayo utaipata ofisi ya Mhasibu utakapofika chuoni. Au wasiliana na Mhasibu kwa namba **0755 265 308** kwa ajili ya kupatiwa Control number. Malipo yanaweza kufanywa kupitia Mawakala wa mitandao ya simu au benki yeyote.

Baada ya malipo uje na nakala ya malipo (Pay Slip) yenye majina yako kamili wakati wa kuripoti chuoni.

**N.B**

Malipo yote yafanyike kwa kutumia **CONTROL NUMBER** uliyopewa na ofisi ya uhasibu **ISIPOKUWA** Tsh **50,400/=** ya Bima ya Afya utajulishwa utaratibu wa kulipa siku ya kuripoti.

***ZINGATIA,*** Ada na malipo mengineyo yote ya muhula wa kwanza yaliyoainishwa hapo chini yanalipwa kwa pamoja kwa kutumia **control number uliyopewa** na si vinginevyo.

5. **SARE YA CHUO KWA WAVULANA NA WASICHANA**

i. Suruali bluu bahari.

ii. Mashati mawili meupe (Mikono mifupi aina ya tomato) ya tetron, jozi ya viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba utapaswa kuvinunua mwenyewe.

**HATA HIVYO, Suruali,sweta na tisheti na utapatiwa chuoni baada ya kulipia.**

Kwa wanafunzi wa fani ya UVUVI watalazimika kununua **gumboot za rangi nyeupe**.



Kwa wanafunzi wa fani za bomba,umeme ,magari na uashi watalazimika kununua **safety boot za rangi nyeusi**.



6. **MAVAZI/ SARE YA MICHEZO**

i. Truck suit ya rangi nyeusi au bluu, na Tshirt yenye nembo ya VETA inapatikana chuoni

ii. Raba rangi yoyote.

**7. MAHITAJI KWA AJILI YA TAALUMA**

i. Mwanafunzi anahitajika kuja na daftali kubwa (8) nane (Counter book Q2)
ii. Set ya vifaa vya kuchorea
iii. Rimu moja ya karatasi nyeupe A4

**8. MAHITAJI KWA AJILI YA MALAZI NA CHAKULA**

i. Wanachuo wa bweni wafike na, mto, shuka mbili za rangi ya bluu au pink/blanketi jepesi, chandarua, bakuli, sahani, kikombe na kijiko, pamoja na ndoo ya kuogea.

**9. MAHITAJI KWA AJILI YA USAFI WA MAZINGIRA**

i. Jembe ii. Fyekeo (slasher)

**10. MAELEKEZO YA ZIADA**

1. Ada ikishalipwa haitarudishwa.
2. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za Chuo kama zilivyo ambatanishwa kwenye barua hii.
3. Nafasi yako kama mwanachuo itapotea endapo utashindwa kuripoti Chuoni wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo.
4. **Utatakiwa kuzingatia vipindi vyote vya masomo vikiwemo vya nadharia na vitendo. Uongozi wa chuo unaweza kuchukua uamzi wa kukusimamisha kuendelea na mafunzo ndani ya kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo, iwapo itathibitika kuwa uwezo wako kimasomo ni mdogo.**
5. Wazazi/ Walezi watunze kumbukumbu za malipo ya ada na mahitaji mengine (Risiti) za malipo hayo na kuziwasilisha (au kumkabidhi Mwanafunzi husika aziwasilishe chuoni siku ya kuripoti chuoni).
6. Muda wa kuripoti chuoni ni siku za kazi Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri.

**JEDWALI LA MCHANGANUO WA MALIPO KWA WANAFUNZI WA FANI ZA** FOOD PRODUCTION (**FP)** NA FOOD AND BEVERAGE SERVICES AND SALES **(FBSS)**

| **NA** | **MAHITAJI** | **KWA WANAFUNZI WA KUTWA (DAY)** | | **KWA WANAFUNZI WA BWENI (BOARDING)** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** |
| 1. | Karo ya mafunzo | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 |
| 2. | Fedha ya Tahadhari (caution money) | 20,000 | | 20,000 | |
| 3. | Kitambulisho | 5,000 | | 5,000 | |
| 4. | Nembo ya VETA | 5,000 | | 5,000 | |
| 5. | Ada ya mtihani wa Taifa | 30,000 | | 30,000 | |
| 6. | Mchango wa mahafali | 10,000 | | 10,000 | |
| 7. | Sare za shule (Suruali mbili) | 50,000 | | 50,000 | |
| 8. | Michezo | 10,000 | | 10,000 | |
| 9. | Sweta Bluu | 25,000 | | 25,000 | |
| 10. | T-shirt | 20,000 | | 20,000 | |
| 11. | Picha (Passport size) | 3,000 | | 3,000 | |
| 12. | Chai | 20,000 | | 0 | |
| 13. | Kukodisha godoro | 0 | | 10,000 | |
| 14. | Sare ya mafunzo ya Huduma kwa wanafunzi wa (FOOD PRODUCTION-**FP** NA FOOD AND BEVERAGE SERVICES AND SALES-**FBSS**) | 75,000 | | 75,000 | |
| | **JUMLA KUU** | **303,000** | **30,000** | **323,000** | **60,000** |

**JEDWALI LA MCHANGANUO WA MALIPO KWA FANI ZA UFUNDI**
MAGARI,UMEME ,UJENZI,USHONAJI NA BOMBA.

| **NA** | **MAHITAJI** | **KWA WANAFUNZI WA KUTWA (DAY)** | | **KWA WANAFUNZI WA BWENI (BOARDING)** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** |
| 1. | Karo ya mafunzo | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 |
| 2. | Fedha ya Tahadhari (caution money) | 20,000 | | 20,000 | |
| 3. | Kitambulisho | 5,000 | | 5,000 | |
| 4. | Nembo ya VETA | 5,000 | | 5,000 | |
| 5. | Ada ya mtihani wa Taifa | 25,000 | | 25,000 | |
| 6. | Mchango wa mahafali | 10,000 | | 10,000 | |
| 7. | Sare za shule (Suruali mbili) | 50,000 | | 50,000 | |
| 8. | Overcoat/overall | 30,000 | | 30,000 | |
| 9. | Sweta Bluu | 25,000 | | 25,000 | |
| 10. | Michezo | 10,000 | | 10,000 | |
| 11. | T-shirt | 20,000 | | 20,000 | |
| 12. | Picha (Passport size) | 3,000 | | 3,000 | |
| 13. | Chai | 20,000 | | 0 | |
| 14. | Kukodisha godoro | 0 | | 10,000 | |
| | **JUMLA KUU** | **253,000** | **30,000** | **273,000** | **60,000** |

**JEDWALI LA MCHANGANUO WA MALIPO KWA FANI YA UVUVI NA UCHAKATAJI SAMAKI.**

| NA | MAHITAJI | KWA WANAFUNZI WA KUTWA (DAY) | | KWA WANAFUNZI WA BWENI (BOARDING) | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** | **MUHULA WA I** | **MUHULA WA II** |
| 1. | Karo ya mafunzo | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 |
| 2. | Fedha ya Tahadhari (caution money) | 20,000 | | 20,000 | |
| 3. | Kitambulisho | 5,000 | | 5,000 | |
| 4. | Nembo ya VETA | 5,000 | | 5,000 | |
| 5. | Ada ya mtihani wa Taifa | 30,000 | | 30,000 | |
| 6. | Mchango wa mahafali | 10,000 | | 10,000 | |
| 7. | Sare za shule (Suruali mbili) | 50,000 | | 50,000 | |
| 8. | Overcoat | 30,000 | | 30,000 | |
| 9. | Sweta Bluu | 25,000 | | 25,000 | |
| 10. | Michezo | 10,000 | | 10,000 | |
| 11. | T-shirt | 20,000 | | 20,000 | |
| 12. | Picha (Passport size) | 3,000 | | 3,000 | |
| 13. | Chai | 20,000 | | 0 | |
| 14 | Kukodisha godoro | 0 | | 10,000 | |
| | **JUMLA KUU** | **258,000** | **30,000** | **278,000** | **60,000** |

**Malipo hayo yanalipwa kwa Control namba utakayopewa Chuoni na si vinginevyo.**

**KARIBU CHUO CHA VETA- CHATO**

……………………………………….

**LILIAN MLIMIRA**

**KAIMU MKUU WA CHUO**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA UFUNDI STADI VETA CHATO**

**TARATIBU NA SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI**

Katika kipindi chote mwanafunzi awapo chuoni atatakiwa kuzingatia sheria na taratibu zifuatazo.

**MUHIMU**

(a) Kila mwanafunzi anapaswa kuwa katika eneo la chuo kabla au ifikapo saa 1.30 asubuhi.
(b) Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya chuo kwa sababu yoyote ile bila ruhusa ya Mwalimu wa zamu.
(c) Ruhusa ya kumlazimu mwanafunzi kulala nje ya chuo, ipitishwe, kwa mwalimu mlezi (Matron /Warden) na Mwalimu wa zamu kabla ya kufikishwa kwa Msajili.
(d) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari zifike chuoni za kutoa taarifa hiyo bila kufanya hivyo ni kosa.
(e) Mahudhurio chini ya 85% yatamsababishia mwanafunzi kukosa cheti cha kumaliza mafunzo (leaving certificate).

**1. MAVAZI**

a) Sare ya Chuo ni suruali ya rangi ya Bluu na shati jeupe la mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni, wakati wa kuja Chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe **limechomekewa**.
b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.
c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandozi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

**2. USAFI WA MWILI**

a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote kwa kipindi chote mwanafunzi awapo chuoni.
b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali
**c) Nywele kwa wavulana**

- Zikatwe ziwe fupi na mitindo kama PANKY, AMERICAN BASE NA KIPARA hairuhusiwi kabisa.
- Ndevu haziruhusiwi.

**d) Nywele kwa wasichana**

- Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mstari (twende kilioni)

NB: Nywele ndefu na nywele zenye kupakwa madawa kama vile carl, raster na golden hair haziruhusiwi kabisa kwa kipindi chote cha mafunzo.

**3. WIZI**

(a) Wizi au vitendo vyovyote vinavyo husishwa na wizi haviruhusiwi, endapo itathibitika kuwa mwanafunzi ameiba au kuhusishwa katika tukio lolote la wizi adhabu yake ni kufukuzwa chuo.
(b) Ukipoteza vifaa vya Chuo utatakiwa kulipa au kufidia gharama kamili ya kifaa kilichopotea ndani ya siku kumi na nne.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya karakana za chuo.
(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini

**4. UGOMVI**

Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Mwanachuo atakayepatikana akijihusisha na vitendo vya nanma hiyo atafukuzwa Chuo na kukabidhiwa kwenye vyombo vya vya mamlaka za kisheria.

**5. ULEVI:**

Iwapo itathibitika kuwa Mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa Chuo mara moja.

**6. MAPENZI**

(a) Uhusiano wa kimapenzi Chuoni kati ya Mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.
(b) Mwanachuo akipata mimba hataruhusiwa kuendelea na masomo.

**7. MIGOMO:**

Migomo au kuchochea migomo ni kosa kwa mujibu wa taratibu na sheria za chuo hiki. Mwanachuo atakayeshawishi, kusababisha au kushiriki migomo atafukuzwa Chuo.

**8. LUGHA**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni Kiingereza na Kiswahili hivyo ni wajibu wa kila Mwanafunzi kuzifahamu lugha hizo.

**9. KUBADILI JINA**

Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili Jina ispokuwa pale itkapothibitika kuwa ni lazima kufanya hivyo, kwa uthibitisho wa kisheria.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI:**

Wanachuo wa bweni wataamka saa kumi na mbili asubuhi na kufanya usafi wa mazingira wanamoishi.

10. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo:
    (i) Jumapili tangu saa 12:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni.
    (ii) Jumamosi tangu saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.

    Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati mwingine wowote bila kibali maalum.

11. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuvaa sare ya Chuo yenye nembo ya VETA. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuvaa sare yenye nembo ya VETA atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa Chuoni.

12. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kubali atafukuzwa chuo.

13. Hairuhusiwi kulala au kuwa ndani ya bweni wakati wa parade asubuhi au wakati wote wa masomo. Ukikutwa bwenini kwa muda huo bila kuwa na kibali adhabu kali itatolewa ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya bweni.

14. Hairuhusiwi kupika wala kupeleka chakula bwenini, endapo kuna mgonjwa ruhusa itatolewa na Mwalimu wa zamu/mlezi wa bweni. Atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua za kinidhamu.

15. (a) Ni marufuku Wanachuo wa Kiume na Wakike kutembeleana mabwenini.
(b) Hairuhusiwi KABISA kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa Chuo bila ya ruhusa.

16. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:30 usiku.
17. Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha au kumlaza mgeni bwenini.
(a) Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.
(b) Kila Jumapili na siku za Sikukuu kuanzia saa 1:00 asubuhi mpaka 11:00 jioni.

18. Vyumba/Madarasa na vifaa vingine vitumiwe kwa kadiri ya matumizi yaliyokusudiwa. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

19. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

20. Ruhusa ya kutoka Chuoni ni: Jumamosi saa 7:00 mchana hadi saa 11.00 jioni. Jumapili na siku za Sikukuu saa 1.00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mwanachuo atapaswa kuandika katika daftari la walinzi getini muda wa kutoka na kusaini arudipo chuoni.

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**
**CHATO DISTRICT VOCATIONAL TRAINING CENTER (CHATO DVTC)**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Admission to CHATO DVTC is conditional upon receipt of satisfactory medical report. The practitioner to whom this form is presented is requested to examine the candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an…………………................. (Trade)

The Medical Officer
……………………………….
……………………………….
……………………………….
……………………………….
Please examine …………………………………………….... (candidates name)

(i) Eyesight………………………………………………
(ii) Hearing……………………………………………….
(iii) Height…………………………………………..…..
(iv) Allergies………………………………………………
(v) Weight……………………………………………….
(vi) Asthma……………………………………………….
(vii) Epilepsy………………………………………………
(viii) Other serious diseases……………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that/she is physically fit/unfit for training as above.
TITLE…………………………………………SIGNATURE………………………..
Official Stamp………………………………… Date…………………………….

AFFIX YOUR PASSPORT SIZE HERE

BANDIKA PICHA YAKO HAPA (Mwanafunzi)

**TAARIFA YA MWANACHUO (PERSONAL PARTICULARS)**
**SEHEMU (A)**

Ijazwe na mwanafunzi (tumia herufi kubwa)
1. Jina la ukoo Bw./Bibi/Bi…………………………………………………………….
2. Majina mengine……………………………………………………………………….
3. Mahali ulipozaliwa (Wilaya)……………………………..Mji/Kijiji…........
4. Kiwango cha elimu………………………
4. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa………………………………………………..
5. Hali ya ndoa………………………(umeoa/olewa)
6. Anuani ya makazi ya kudumu……………………………………………………..
7. Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………….
8. Anuani ya mzazi/mlezi……………………………………………………….....
9. Namabri ya simu ya mzazi/mlezi…………………………………………………

**Uthibitisho**

Mimi ………………………………………………… Nathibitisha kwamba, ninaikubali nafasi hii, na kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi na za kweli.

Sahihi………………………………… Tarehe…………………………………

**SEHEMU (B)**

Ijazwe na Mzazi/Mlezi/Mdhamini

Mimi …………………………………… S.L.P. ……………………………………………

Simu ya mkononi……………………………………………

Ninathibitisha kuwa ninamdhamini mtajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za Mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo.

Tarehe…………………………... Sahihi……………………………………

Uhusiano………………………………………………………………